TANGAZO LA SERIKALI NO. 806 La Tarehe 28/12/2018

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA. NA. 272)

———

AMRI

———

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (1)(d))

———

AGIZO LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MPWAPWA ("MPWAPWA WSSA"), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2018

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpwapwa("Mpwapwa WSSA"), (la Kurekebisha Bei), la Mwaka 2018.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Desemba 2018.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Mpwapwa WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 28Februari 2019 au kabla, Mpwapwa WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo

hili;

(b) Mpwapwa WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili;

(c) Mpwapwa WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

(d) MpwapwaWSSA itahakikisha kuwa taarifa zake za fedha zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) au mtu yeyote aliyeidhinishwa kutokana na kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kuhakikisha inawasilisha EWURA rasimu za mahesabu yaliyokaguliwa;

(e) Ifikapo tarehe 30 Mei 2019 au kabla, Mpwapwa WSSA itafanya tathmini ya thamani ya mali zakena kuwasilishaEWURAtaarifayatathmini iliyothibitishwa na Mtathmini aliyesajiliwa;

(f) Mpwapwa WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(g) Mpwapwa WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mpwapwa WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote

yatakayowasilishwa naMpwapwa WSSA katika siku zijazo; na

(h) Kuanzia tarehe 1 Desemba 2018, Mpwapwa WSSA itaanza kulipa tozo ya EWURA kwa mujibu wa kifungu namba 43 cha Sheria ya EWURA, Sura 414 nakifungu namba 6 cha Kanuni za EWURA kuhusu Taratibu za Kukusanya ada na tozo zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali namba193 la mwaka 2010.

Utenguzi wa Agizo Na. 16-012 la tarehe 1 Juni 2016

5. Agizo hili linatengua Agizo La Mapitio ya Bei Na. 16-004 la tarehe 1 Februari 2016 katika maeneo yanayohudumiwa na Mpwapwa WSSA.

_____

Majedwali

_____

JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Matumizi	Bei ya Sasa 2017/18	Bei Ziliyoidhinishwa		
			2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	0-10	630	640	650	660
	>10	1,045	1,060	1,080	1,085
Taasisi	0-10	1,285	1,410	1,430	1,435
	>10	1,565			
Biashara	0-10	1,325	1,560	1,590	1,600
	>10	1,605			
Viwanda	1	NA	1,065	1,090	1,090
Magati	1	1,000	1,000	1,000	1,000
WAT		1020.37	1039.51	1055.66	1061.42

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	2,500	Imeondolewa		
Biashara	4,000			
Taasisi	4,000			
Viwanda	0			

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	Asilimia ishirini ya gharama ya vifaa	Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyoelezwa katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013		
Biashara				
Taasisi				
Viwanda				

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	15,000	20,000	20,000	20,000
Biashara	20,000	25,000	25,000	25,000
Taasisi	20,000	25,000	25,000	25,000
Viwanda	0	25,000	25,000	25,000

JEDWALI LA PILI
MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

Maelezo ya Kazi zitakazofanyika	Gharama (Shilingi)			Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji
	2018/19	2019/20	2020/21	
Ukarabati na Ubadilishaji Miundombinu ya Zamani				
Kubadilisha bomba chakavu za kwenye kisima na vipuli vya kuwashia pampu.		3,000,000		Ifikapo tarehe 30 Juni, 2020
Kukarabati chanzo cha maji kilichopo Mayawile kwa kuboresha mlango wa maji na mabomba yaliyopo.		5,000,000		Ifikapo tarehe 30 Juni, 2020
Kuboresha mfumo wa kutibu maji	500,000			Ifikapo tarehe 30 Juni, 2019
Kubadilisha bomba chakavu za chuma urefu wa km.6 zenye kipenyo cha mm.80 na mm.100	60,500,000		63,525,000	Ifikapo tarehe 30 Juni 2019; Ifikapo tarehe 30 juni,2021
Kubadilisha valvu za kufunga maji zilizopo Igovu (2, mm.100), Mazae(1,mm.100) na Ilolo(1, mm.100)	3,080,000			Ifikapo tarehe 30 Juni, 2019
Kubadilisha valvu za kutoa hewa zilizopo Mazae (1, mm.50), Ilolo(1, mm.100) and Mji Mpya(1, mm.50)	1,870,000			Ifikapo tarehe 30 Juni, 2019
Kubadilisha bomba chakavu za chuma maeneo ya Mazae, km. 1 na Ilolo km.2 (mm. 90 na mm.63, polypipes,PN10)	33,000,000	16,500,000		Km.2kmIfikapo tarehe 30 Juni, 2019 ; Km. 1Ifikapo tarehe 30 Juni, 2019 2020.
Kubadilisha dira za maji chakavu iliyopo tanki la igovu(mm. 200,Class C) at Igovu storage tank	5,000,000			Ifikapo tarehe 30 Juni, 2019 2020.

Kubadilisha dira za maji chakavu iliyopo tanki la zamani katika eneo la Igovu (mm. 100,Class C)		2,500,000		Ifikapo tarehe 30 Juni, 2020.
Kubadilisha dira za maji chakavu za wateja (dira 200 kila mwaka, mm. 15,Class C)	19,800,000	20,790,000	21,829,500	Dira 200 kila mwaka 200,
Kubadilisha samani za ofisi- viti(5), meza (2), makabati (4)		1,350,000	2,600,000	Viti(5), meza (2)Ifikapo tarehe 30 Juni, 2020 ; Makabati (4) Ifikapo tarehe 30 Juni, 2021
JUMLA YA GHARAMA – UKARABATI NA UBADILISHAJI MIUNDOMBINU YA ZAMANI	123,750,000	49,140,000	87,954,500	
Miradi Mipya				
Upanuzi wa mtandao wa usambazaji urefu wa km.4.5. Mazae (km.2, mm.63, PN10) takribani wateja wapya100, Majumba Sita (km.1.5, mm. 63, PN10) takribani wateja wapya 50 na Chinyika (km 1, mm.63,PN10) takribani wateja wapya 50	20,900,000	10,972,500	15,112,125	Mazae km.2 ifikapo tarehe 30Juni 2019; Chinyika km.1 ifikapo tarehe 30Juni 2020; Majumba Sita km.1.5, ifikapo tarehe 30Juni 2021.
Kuchimba kisima kirefu eneo la kikombo			18,600,000	Ifikapo tarehe 30 Juni 2021
Kujenga nyumba kwa ajili ya mitambo ya kusuma maji, Kikombo			15,000,000	Ifikapo tarehe 30 Juni 2021
Kununua pampu yenye uwezo wa (Q=40m3/hr, H=120m, and Motor Control Centre (MCC))			40,540,080	Ifikapo tarehe 30 Juni 2021
Upanuzi wa bomba kuu la usafirishaji maji Kikombo 2 (DN100mm, PN16)			6,966,667	Ifikapo tarehe 30 Juni 2021

Ununuzi wa dira za wateja wa maji wa majumbani (210 kila mwaka ,DN15mm, Daraja C); biashara (3 mwaka wa 1, 5 mwaka wa pili 2 na 5 mwaka wa 3,DN15mm, Daraja C); taasisi (21mwaka wa 1, 24 mwaka wa 2 and 4 mwaka wa 3,DN15mm, Daraja C); viwanda (2 mwaka 1, 5 mwaka 2 and 5 mwaka wa 3,DN15mm, Daraja C);	23,364,000	24,354,000	22,176,000	Ifikapo tarehe 30 Juni 2021
Kununua dira 50 za malipo ya kabla (prepaid water meters) (DN15mm,Class C)	3,750,000	7,875,000	8,268,750	Ifikapo tarehe 30 Juni 2021
Kununua dira kwa ajili ya chanzo maji kilichopo Mayawile (DN100mm,Class C)	2,500,000			Ifikapo tarehe 30 Juni 2019
Kununua gari (Station Wagon -3000cc) na pikipiki 4 (150cc)	40,000,000	40,000,000	90,000,000	Ifikapo tarehe 30 Juni 2021
JUMLA YA GHARAMA ZA UWEKEKEZAJI MIRADI MIPYA	90,514,000	83,201,500	216,663,622	
JUMLA KUU YA GHARAMA ZA UWEKEZAJI	214,264,000	132,341,500	304,618,122	

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2018/19	2019/20	2020/21
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	Na	236	245	225
Kiwango cha upotevu wa maji	%	28	28	28

Wateja wenye Dira	%	100	100	100
Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	%	80	81	82
Kiwango cha Mwitikio wa Malalamiko ya Maandishi	%	100	100	100

Dar es Salaam
30 Oktoba 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu